WATEULE

WA

MUNGU

Bibi E. G. White

# WATEULE

# WA

# MUNGU

Na Bibi E. G. White

Mfasiri:  M. Mwamalumbili

The Elect of God - Kiswahili

Wateule  wa  Mungu

"Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.... kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo.  Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa.  Katika yeye huyo, kwa damu yake tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.  Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi;  akiisha kutujulisha siri ya

mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo; na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake" (Waefeso 1:2,4-11).